



## Le Symbole d'Athanase en langue kiswahili

### Imani ya Athanasio

Killa atakae kuokoka: zaidi ya yote imemlazimu kuishika Imani Katholiko.

Nayo asipoilinda pasipo kuipunguza wala kuiharibu: bila shaka atapotea milele.

Na Imani Katholiko ni hii: tumwabudu Mungu minoja katika Utatu, na Utatu katika Umoja; Tusizichanganye nafsi: wala kuigawanya asili.

Kwa maana nafsi ya Baba mbali, nafsi ya Mwana mbali: nafsi ya Koho Mtakatifu mbali.

Bali Uungu wa Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu ni Uungu umoja: Uttikufu wao sawa, Ukuu wao wa milele.

Kama alivyo Baba, ndivyo alivyo Mwana: ndivyo alivyo Roho Mtakatifu.

Baba hakuumbwa, Mwana hakuumbwa: Roho Mtakatifu hakuumbwa.

Baba hana mpaka, Mwana hana mpaka: Roho Mtakatifu hana mpaka.

Baba wa milele, Mwana wa milele: Roho Mtakatifu wa niilele.

Walakini hakuna watatu walio wa milele: illa Mmoja aliye wa milele.

Kadhalika hakuna wata'tu wasioumbwa, wala watatu wasio na mpaka: illa mmoja tu asiyeumbwa, na mmoja tu asiye na mpaka.

Kadhalika Babani Mwenyiezi, Mwana ni Mwenyiezi: na Roho Mtakatifu ni Mwenyiezi.

Bali hakuna Watatu walio Wenyiezi: illa aliye Mwenyiezi ni mmoja tu.

Yivyo hivyo Baba ni Mungu, na Mwana ni Mungu: na Roho Mtakatifu ni Mungu.

Bali hakuna Miunguwatatu: illa Mungu mmoja tu.

Vivyo bivyo Baba ni Bwana, na Mwana ni Bwana: na Roho Mtakatifu ni Bwana.

Bali hakima Bwanawatatu: illa Bwana mmoja tu.

Kwa maana kama tunavyoshurutishwa kwa kanuni ya kweli ya Kikristo: kukiri ya kuwa killa nafsi ni Mungu na Bwana;

Kadbalika tunagombezwa na Imani Katholiko: tuiseme ya kuwa wako Miungu watatu au Bwana watatu.

Baba hakuumbwa na aliye yote: wala hakukhulukiwa wala hakuzaliwa.

Mwana anatoka katika Baba tu: bakuumbwa, wala hakukhulukiwa, bali anazaliwa.

Roho Mtakatifu anatoka katika Baba na katika Mwana: hakuumbwa, wala hakukhulukiwa, wala hakuzaliwa, bali anatoka.

Bassi yupo Baba mmoja tu, si Baba watatu; yupo Mwana mmoja tu, si Wana watatu: yupo Roho Mtakatifu mmoja tu, si Roho Watakatifu watatu.

Na katika Utatu huu hapana aliye wa kwanza na aliye wa baadae: hapana aliye mkuu zaidi na aliye

mdogo.

Bali nafsi zote tatu ni wa milele: wa sawa wote.

Bassi katika mambo yote kama tulivyokwisha kusema: imetulazimu kuuabudu Umoja katika Utatu, na Utatu katika Umoja.

Bassi ye ye atakae kuokoka: audhanie hivi Utatu.

Na zaidi ya haya, apate wokofu: imemlazimu kukuamini kwa moyo Kufanyika mwili kwake Bwana wetu Yesu Kristo.

Na Imani kamili ndiyo hii: tuamini, tukiri ya kuwa Bwaiia wetu Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, ni Mungu na Mwana Adamu.

Ni Mungu, ana asili ya Baba, amezaliwa kabla ya zamani zote: ni Mwana Adamu, ana asili ya Mama wake, alizaliwa katika zamani.

Mungu kamili na Mwana Adamu kamili: ana roho yenye akili na mwili wa Mwana Adamu.

Yu sawa na Baba kwa kuwa ni Mungu: Yu chini ya Baba kwa kuwa ni Mwana Adamu.

Na ijapokuwa yu Mungu na Mwana Adamu: ye ye si wawili illa Kristo mmoja.

Yeye ni mmoja, si kana kwamba Uungu urnebadilika uwe mwili: bali kwa kuitwaa asili ya Mwana Adamu na kuiunga na Uungu.

Mmoja kabisa; si kwa kuzichanganya asili zile mbili: bali kwa kuwa Nafsi mmoja tu.

Kwa maana karaa roho yenye akili pamoja na mwili huwa Mwana Adamu mmoja: kadhalika Mungu na Mwana Adamu pamoja ni Kristo mmoja;

Aliyeteswa kwa wokofu wetu: akashuka mahali pa wafu, akafufuka siku ya tatu.

Akapaa mbinguni, anaketi mkono wa kuume wa Mungu Baba Mwenyeze: kutoka huko atakuja kuwashukumu watu wahayi na wafu.

Atakapokuja ye ye, wana Adamu wote watafufuka na miili yao: watatoa khabari za matendo yao.

Nao waliotenda mema wataingia katika uzima wa milele: nao waliotenda mabaya katika moto wa milele.

Hii ndiyo Imani Katholiko: killa mtu asiyekubali kwa moyo hawezi kuokoka.

Utukufu una Baba, na Mwana: na Koho Mtakatifu;

Ulivyokuwa mwanzo: ulivyo sasa, utakavyokuwa milele. Amin.

---

Reproduit avec l'aimable autorisation de [l'Église protestante réformée](#) de Ballimena, en Irlande du Nord, au Royaume-Uni.

[www.ressourceschretiennes.com](http://www.ressourceschretiennes.com)



2022. Utilisé avec permission. Cet article est sous licence Creative Commons.

Paternité – Partage dans les mêmes conditions 4.0 International ([CC BY-SA 4.0](#))